## AckySHINE.com

# Faida ya kuabudu Ekaristi Takatifu

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · February 27, 2020

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Ekaristi Takatifu · #Katoliki: Kuabudu kwa Mkatoliki · #Katoliki: Mwili na Damu ya Yesu

1.Kila saa moja tunayotumia kuabudu, inafurahisha moyo wa Yesu na hivyo majina yetu huandikwa mbinguni kwa ajili ya uzima wa milele (Mama Thereza wa Calcuta)

2.Maisha ya kiroho ya familia zetu yanaimarishwa kwa njia ya saa ya kuabudu (John Paul II)

3. Saa takatifu ya kuabudu ni ya muhimu sana kiasi kwamba roho za waamini wengi huenda kwenye uzima (mbinguni) badala ya motoni (ufunuo wa Yesu kwa Dina Belanger)

4. Wakati pekee ambao Yesu aliwaomba kitu wanafunzi wake ni wakati anakaribia mateso na hakuomba chochote isipokua saa moja ya kukesha nae (Askofu Mkuu Fulton Sheen)

5.Saa moja takatifu ya kuabudu ni kushiriki katika harakati za ukombozi (Askofu mkuu Fulton Sheen)

6. Neema ya kuabudu Ekaristi iko juu ya watu wote (St Peter Julian Eymard)

7.Bwana wetu Yesu husikia maombi yetu yote na popote lakini amewafunulia watu wake kuwa wale watakaokwenda kukaa nae katika kuabudu Ekaristi wanapata neema zaidi (Mtakatifu Alphonsus Ligoria)

8.Kila saa unapokwenda kuabudu kumbuka kwamba Yesu amekusubiria wewe binafsi kwenda kumtembelea kwa karne ishirini (St Josemaria scavia)

9.Kuabudu kwa dhati kuna neema na manufaa makubwa ambayo huzidi kwa wale wanaoabudu, hupanuka na kugusa nyumba zao familia zao na mpaka katika parokia zao (Pope Paul VI)

10. Saa moja takatifu mbele ya Ekaristi ni muhimu kuliko miaka elfu moja ya utukufu wa mwanadamu (Mtakatifu Padre Pio)